Barry, A. L. - WHAT ABOUT? ABORTION - Swahili

Kuhusu Jambo Gani...

# Kutoa Mimba/ Kuavya

**Daktari A. L. Barry**
**Rais**
**Kanisa la Kilutheri la Sinodi ya Missouri**

## Kuna Nini Kuhusu Kutoa Mimba?

Kutoa mimba ni mojawapo ya masuala nyeti sana ya kimaadili ya wakati huu wetu. Mihemuko huingia mioyoni jambo hili linapotokea. Ni majaribu kuliona suala hili kutoka kwa mtazamo wa viwango vyetu vya tamaduni. Wakristo wanataka wajulishwe juu ya kutoa mimba kutoka kwa Neno la Mungu.

## Neno la Mungu Husema Nini juu ya Kutoa Mimba?

Amri ya Tano ya Mungu ni wazi, "Usiue." Katika maneno ya Katekisimo Ndogo, maana yake ni: "Imetupasa kumwogopa na kumpenda Mungu, ili tusiyahatarishe maisha ya jirani yetu wala tusimwumize [au tusimdhuru], ila tumsaidie na kumstawisha katika kila haja ya maisha." Mungu hutukataza tusiutoe uhai wa mtu mwingine, na kwa hakika hii ni pamoja na kutoa mimba.

Vile vile Neno la Mungu husema, "Kabla sijakuumba katika tumbo nalikujua, na kabla hujatoka tumboni, nalikutakasa" (Yer. 1:5). Zaburi 139:16 husema, "Macho [Y]ako yaliniona kabla sijakamilika, Chuoni [M]wako ziliandikwa zote pia, Siku zilizoamriwa kabla hazijawa bado."

Maelezo ya kanisa letu katika Katekisimo Ndogo hulielezea suala hili vizuri yanaposema, "Walio hai lakini hawajazaliwa ni wanadamu mbele za Mungu tangu wakati walipochukuliwa mimba. Kwa kuwa kutoa mimba huhatarisha maisha ya mwanadamu, si uchaguzi wa kimaadili isipokuwa kwa kuzuia kifo cha mtu mwingine, yaani, mama." Kutoa mimba makusudi, isipokuwa iwe wakati wa dharura ambapo unaweza kuwa lazima, ni kutenda dhambi, ambako ni kinyume kabisa na mapenzi ya Mungu.

## Kanisa Linawezaje Kupinga Kutoa Mimba ikiwa ni Halali huko Amerika?

Licha ya kwamba, tendo fulani ni halali kisheria, haliwi lenye maadili, jema au sahihi. Huenda kutoa mimba kukawa mojawapo ya mfano wa kuvutia wa hali ambayo tendo fulani ni halali, lakini ni dhambi hasa mbele za Mungu. Tangu mwaka wa 1973, kutoa mimba kulihalalishwa huko Amerika. Kutoa mimba hubaki kuwa dhambi mbele za Mungu, kuwe halali au kusiwe katika jamii zetu. Kwa hiyo, lazima "kumtii Mungu kuliko wanadamu" (Matendo ya Mitume 5:29). Kanisa linahitaji kuwajulisha washiriki wake kwamba, kutoa mimba ni dhambi na kisha kuwatia moyo, kama wananchi Wakristo, kutumia njia za kisheria zilizopo kuzibadilisha sheria. Wakristo hawatumii matendo yaliyo kinyume cha sheria kubadilisha sheria za nchi.

## Kwa Nini Kanisa Lijihusishe Lenyewe katika Maamuzi ya Mtu Binafsi?

Maamuzi ya mtu binafsi si lazima yawe ya siri. Kanisa pamoja na wachungaji wake, kwa njia mamlaka yote, wamepewa majukumu na Mungu kuonya, kukaripia na kukemea kutoka kwa Neno la Mungu (2 Tim. 4:2). Kanisa linasikitika sana Wakristo wanapofanya maamuzi yaliyo kinyume cha Neno la Mungu na kwa hiyo, wenyewe hujifungia nje ya mapenzi ya Mungu. Kuishi katika dhambi isiyosameheka ni hatari sana. Kwa hiyo, kanisa lazima liwaonye washiriki wake dhidi ya majaribu ya kutoa mimba. Kanisa pia lazima liwahudumie wale waliokwisha kutoa mimba. Isitoshe, linahitaji kuipinga dhambi ya kutoa mimba, kwa kuwa katika tamaduni zetu, linaonyeshwa kama tendo linalokubalika sana.

**Kanisa la Kikristo Limekuwa Likipinga Kutoa Mimba daima?**

Kutoa mimba kulikuwa jambo la kawaida wakati wa utawala wa kale wa Warumi. Ukweli kwamba, Mwana wa Mungu alichukuliwa mimba katika tumbo la Bikira Mariamu, ulikuwa sababu yenye nguvu kwa Wakristo kuuthamini sana uhai wote wa binadamu. Aliyekuwa hajazaliwa, Kristo, hakuwa tu kibonge cha seli (a blob of cells) bali kwa kweli alikuwa Mwana wa Mungu, ambaye alikuwa ameichukua asili ya binadamu ili kuwaokoa na kuwakomboa wanadamu kutoka kwa dhambi zao. Waandishi Wakristo wa kale huweka wazi kwamba, kutoa mimba kulikuwa chukizo kwa Wakristo wa kwanza. Wakristo hao walijua mitazamo yao juu ya ndoa, ya wanawake na ya familia kuwa ya pekee. Baba mmoja wa kanisa alisema waziwazi, "Tofauti ya kuogofya baina ya kilichoumbwa na ambacho hakijaumbwa ni mamoja kwetu. Yeyote atakayetoa mimba makusudi astahili adhabu ya mauaji ya binadamu." Kutoka mwanzo, kanisa la Kikristo limekuwa likipinga kutoa mimba, likikuchukulia kama mauaji ya watoto wachanga (infanticide) na kama mauaji ya binadamu (homicide).

**Kwa Nini Makanisa Mengine Huyumbayumba Kuhusu Suala la Kutoa Mimba?**

Kutoa mimba ni tendo la kusikitisha na linalowatisha sana watu wengi. Ni rahisi kwa kanisa kuchukua msimamo hafifu na kutokataa waziwazi ubaya wa kutoa mimba. Hata hivyo, makundi ya makanisa yanayotaka yawe na yabaki kuwa maaminifu kwa Maandiko Matakatifu hayawezi kunyamaza bali lazima yaonyeshe wazi kwamba, kutoa mimba makusudi ni dhambi. Madhehebu mengi makuu yasiyopendelea upande wowote, ambayo huvumilia kutokuamini na kupuuza mafundisho mengi ya Biblia katika makanisa yao, huvumilia pia na hata hutetea kutoa mimba. Mara nyingi hali hii huwakanganya Walutheri wa Sinodi ya Missouri wanaposikia kwamba, baadhi ya makanisa mengine ya Kilutheri hayachukui msimamo imara kuhusu kutoa mimba. Ni muhimu sana kwetu kudhihirisha kwamba, kanisa letu haliungi mkono msimamo wa makundi hayo ya makanisa ambayo hayapingi waziwazi dhambi ya kutoa mimba.

**Si Kutoa Mimba Kunakubalika Mimba Inapotokana na Kubakwa au Kujamiiana (incest)?**

Ingawa mabishano ya kusikitisha juu ya kutoa mimba katika hali hizi [mbili] yanaweza kuonekana kuwa ya lazima, ukweli ni kwamba, ni makosa kuutoa uhai wa mtu asiyekuwa na hatia (mtoto ambaye hajazaliwa), na kwa njia hiyo, kumtwika mzigo mtu mwingine aliyejihusisha na hali hii ya kutisha, yaani, mama. Kwa kweli ni mantiki (logic) ya ajabu itakayotufanya tumuue mtoto asiyekuwa na hatia ambaye hajazaliwa kwa dhambi ya babake.

**Tunaweza Kuwafanyia nini Watu Wanaopanga Kutoa Mimba?**

Ni dhambi kwa wazazi kuwashauri watoto wao kutoa mimba. Hii si hiari kwa wazazi Wakristo. Mimba isiyopangwa huja kama mshtuko kwa wote wanaohusika na kutoa mimba kunaweza kuonekana kuwa njia "ya haraka na ya siri" ya kuepukana na shida hiyo, lakini sivyo. Inazidisha dhambi iliyokwisha kutendwa kwa uchaguzi mwingine wa dhambi.

Msichana au mwanamke apangaye kutoa mimba ana hiari ya kumlea mtoto wake au kumtoa kwa ajili ya upangaji mwana (adoption). Upangaji mwana ni hiari nzuri, kwa kuwa humruhusu mtoto ambaye, vinginevyo, hangeweza kupata malezi bora, kupata upendo na malezi

anayoyahitaji katika familia ambayo inaweza kumlea. Wachungaji wetu wanafahamu mashirika mengi yanayoshughulikia upangaji mwana.

**Kanisa Linawezaje Kuwahudumia Waliokwisha Kutoa Mimba?**

Mwanzoni, msichana au mwanamke aliyekwisha kutoa mimba anaweza kuhisi kwamba, ameiepuka "shida" yake. Mbia (partner) wake, awe rafikiye wa kiume au mumewe, anaweza pia kuhisi kwamba, "amekuwa huru." Karibuni, matokeo yanaweza kuonekana, au huenda yasionekane mpaka baada ya miaka fulani, ambapo watatambua walilolitenda hasa: waliutoa uhai wa mwanao aliyekuwa hajazaliwa. Labda utambuzi huu huja wanapolisikia Neno la Mungu likifafanuliwa kwa usahihi wake kuhusu suala hili. Sheria ya Mungu huifunua dhambi yao na wanajihisi kuwa wenye dhambi na wenye mateso makubwa, na wanaanza kushangaa watakalolifanya juu ya tendo hilo au kama kuna tumaini lolote kabisa.

Msichana au mwanamke aliyekwisha kutoa mimba anahitaji kusikia kwamba, damu ya Yesu Kristo ilimwagika kwa ajili ya dhambi hii pia, na kwamba, katika Yeye, sasa, kuna msamaha kamili na wa bure. Uthabiti (assurance) huu unahitaji kutolewa tena na tena; yaani, kwamba, katika Yesu Kristo kuna msamaha – msamaha kamili na wote. Hivyo ndivyo kanisa huwahudumia wale wanaoendelea kuhisi mzigo wa dhambi ya kutoa mimba, kwa kuwaonyesha msalaba wa Bwana wao Yesu Kristo tena na tena na kuwahakikishia msamaha kamili na wa bure ambao alimshindia kila mmoja msalabani kwa ajili ya dhambi zote.

Basi, ni muhimu kwamba, watu waliokwisha kutubu dhambi yao waendelee kumkaribia Bwana wao kwa njia ya kuhudhuria kanisa kwa uaminifu ambapo wataendelea kusikia Injili ikihubiriwa na ambapo watashiriki Chakula cha Bwana mara kwa mara. Kuungama dhambi kwa siri na kutangaziwa ondoleo la dhambi na mchungaji wao ni njia nyingine yenye uwezo ambayo kwayo Mungu hutoa neema, msamaha na amani Yake kwa mtu anayejihisi kuwa mwenye dhambi juu ya dhambi ya kutoa mimba. Neema na upendo wa Mungu ni vyenye nguvu kuliko udhaifu wowote wa binadamu na damu ya Yesu Kristo hutusafisha dhambi yote (1 Yohana 1:7). Hakika hizi ni Habari Njema na lazima wenye dhambi wote waweze na washiriki habari hizo.

**Unaweza kutuandikia kwa:**

**LUTHERAN HERITAGE FOUNDATION AFRICA, P. O. Box 521, 00502, KAREN, NAIROBI.**

Daktari A. L. Barry
Rais
Kanisa la Kilutheri la Sinodi ya Missouri